

UKWELI UNAPASHWA KUJUA.

SASA
INAPATIKANA
KWA WATU
WAZIMA, WATOTO
NA WATOTO
WACHANGA

MLINDE MTOTO WAKO.



LINDA JAMII YAKO.

Watoto na vijana watakuwa salama watakapopokea chanjo.

Chanjo inawalinda watu wote, wakiwemo watoto na vijana, dhidi ya kuambukizwa COVID-19. Chanjo pia inawazuia watoto na vijana wasidhohofike zaidi wanapokuwa wagonjwa.

Kuna aina mpya za maambukizi ya COVID-19, ikijumuisha Delta, ambayo huenea kwa urahisi zaidi na inaweza kusababisha dalili kali zaidi. Chanjo hukulinda dhidi ya aina kama vile Delta.

Chanjo ya watoto na vijana inalinda jamii nzima.

Mtu anapopewa chanjo, ni vigumu kwa mtu huyo kuwasambazia wengine COVID-19. Mtoto aliyefikisha umri unaohitajika anapopewa chanjo inalinda:

- Familia na marafiki zao ambao bado hawajapata chanjo.
- Wakongwe na watu wenye matatizo ya kiafya ambao wako katika hatari kubwa ya kuugua sana wanapokambukizwa COVID-19.

Kadri watoto na watu wazima wanavyoendelea kupata chanjo, itakuwa rahisi pia kuendeleza masomo shuleni na shughuli za kibiashara.



SALAMA NA MADHUBUTI

- Hakuna chanjo nyingine ambayo usalama wake umechunguzwa zaidi ya chanjo hii nchini Marekani.
- Chanjo hii imethibitishwa kuwa salama kwa watoto, vijana na watu wazima, ikiwemo kwa watu wa jamii, kabila na umri mbalimbali.
- Hakuna ushahidi kuwa chanjo zitamfanya mtoto wako asiweze kupata watoto wake mwenyewe.

INATOLEWA BILA MALIPO KWA WATU WOTE

- Wewe na mtoto wako mnaweza kupokea chanjo ya bila malipo pasipo kujali **hali ya uhamiaji**.
- Wewe na mtoto wako hamuhitaji **kuonyesha kitambulisho** au kuwa na **bima ya afya** kupokea chanjo ya bila malipo.

Cha kutarajia

Mtoto wako anapopewa chanjo ya COVID-19, atakuwa salama na anaweza kuendelea na shughuli za kawaida kama kwenda shuleni, kucheza michezo na kutembelea marafiki na familia.



Unapokwenda kupokea chanjo:

- Kabla ya muuguzi au daktari kumpa mtoto wako chanjo, atakueleza kuihusu, ataangalia historia ya matibabu ya mtoto wako na ikiwa una swali atakupea fursa ya kuuliza.
- Mtoto wako atahitajika kusubiri kwa dakika 15-30 ili kuhakikisha kuwa hana mzio wa chanjo.



Athari ni kawaida

Athari HAZIMAANISHI kuwa mtoto wako ana COVID-19.

Athari zinamaanisha chanjo inafundisha mwili wa mtoto wako jinsi ya kupambana na COVID-19.

Athari zisizo kali zinaweza kujumuisha:

- Maumivu au uvimbe kwenye mkono sehemu inayodungwa sindano
- Uchovu
- Maumivu ya kichwa
- Maumivu ya misuli
- Kuhisi baridi
- Joto jingi
- Kuhisi kutapika



Athari kali ni nadra sana

Chanjo ni salama. Kuna uwezekano mkubwa kuwa mtoto wako ataugua zaidi kutokana na maambukizi ya COVID-19 kuliko kutokana na chanjo.

Idadi ndogo ya vijana wamepata athari kama vile moyo kuvimba (inayojulikana kama 'myocarditis' au 'pericarditis') au damu kuganda.

- Athari kali ni **nadra sana**
- Athari kali **zinatibika** na watu wengi walio nazo hupata nafuu
- Chanjo ina faida zaidi kuliko madhara

WASILIANA NA DAKTARI WAKO ILI UPATE MAELEZO ZAIDI

Zungumza na daktari au muuguzi wa mtoto wako ili upate maelezo zaidi kuhusu chanjo za COVID-19 na chanjo zingine ambazo huenda mtoto wako anahitaji.



Kwa maelezo zaidi: cdc.gov/coronavirus